

Simu: +25587719282
Nukushi: +25587866778
Dodoma.



Ofisi ya Makao Makuu
S.L.P 613,
DODOMA
06 Machi 2026

UMOJA WA VIJANA WA CCM (UVCCM)

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UPOTOSHAJI DHIDI YA CHUO CHA MAFUNZO CHA UVCCM IHEMI – IRINGA

Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) tunapenda kuwajulisha watanzania na wadau wote wa maendeleo kuwa kumekuwa na taarifa zinazosambaa katika mitandao ya kijamii zenye madai ya upotoshaji mkubwa dhidi ya Chuo cha Mafunzo cha UVCCM Ihemi, kilichopo Mkoa wa Iringa.

Taarifa hizo zinadai kwamba baadhi ya vijana wa vyama vingine vya siasa wameshikiliwa na kuteswa ndani ya chuo hicho. UVCCM tunasisitiza kuwa taarifa hizo hazina msingi wowote wa ukweli, ni za uongo na ni sehemu ya propaganda yenye dhamira mbaya ya kuchochea chuki na kuvuruga mshikamano wa taifa letu.

Ni muhimu kufahamu kuwa Chuo cha Mafunzo cha UVCCM Ihemi ni taasisi ya mafunzo yenye malengo ya kuwajengea vijana uwezo katika nyanja mbalimbali za uongozi, uzalendo, maadili mema, na ujasiriamali. Chuo hiki kimeanzishwa kwa lengo la kuwaandaa vijana kuwa raia wema, viongozi bora, na wazalendo wanaochangia maendeleo endelevu ya Taifa letu.

Kwa msingi huo, chuo hiki ni kitovu cha mafunzo na maendeleo ya vijana, sio mahali pa vitendo vya ukiukwaji wa haki za bina-damu kama inavyodaiwa kwenye taarifa za upotoshaji zinazo-sambazwa mitandaoni. UVCCM inasisitiza kuwa hakuna vijana wa vyama vingine vya siasa wanaoshikiliwa au kuteswa, na tuhuma zinazotajwa ni za uongo na zinapaswa kuzipuuza.

Tunatoa wito kwa vijana wenzetu na wananchi kwa ujumla kuwa Tanzania ni nchi iliyojengwa juu ya misingi ya amani, umoja, mshikamano na mshikamano wa kitaifa. Tofauti za kisiasa hazipaswi kuwa chanzo cha chuki, uhasama au kusambaza taarifa zisizo na uthibitisho, kwani kufanya hivyo kunaweza kuharibu sifa za taasisi, kuvuruga utulivu wa jamii, na kudhoofisha mshikamano wa taifa letu.

Tujiepushe na upotoshaji, tushirikiane kudumisha amani na kuenzi mshikamano wa Taifa letu.

KULINDA NA KUJENGA UJAMAA

Imetolewa Na:

Idara ya Uhamasishaji na Chipukizi UVCCM - Taifa

6 Machi 2026 | Dodoma.

UKURASA 2/2